

MASWALI YA CHANJO YA COVID-19

Michigan.gov/COVIDvaccine



Je, nitahitaji kukaa katika karantini na kutohudhuria kazini baada ya kupata chanjo?

Kupata chanjo hakuhitaji kukaa katika karantini, lakini kwa kawaida inachukua wiki chache kwa mwili kujenga mwitiko wa kinga baada ya kupata chanjo. Hii inamaanisha kuna uwezekano wa wewe kupata maambukizi ya COVID-19 kabla tu au baada tu ya kupata chanjo. Iwapo unaamini umekuwa katika hatari au una dalili unapaswa kukaa katika karantini hadi utakapozungumza na daktari wako na kupata kupimwa. Usifanye kazi hadi utakapopata majibu yako na kukamilisha muda wa kukaa katika karantini.